

**336/1**  
**LUGHA NA**  
**FASIHI YA KISWAHILI**  
**Paper 1**  
**Oct./Nov. 2025**  
**2 hours**



**UGANDA NATIONAL EXAMINATIONS BOARD**

**Uganda Certificate of Education**

**LUGHA NA FASIHI YA KISWAHILI**

**Karatasi ya Kwanza**

**(Uandishi wa Insha na Ufupisho)**

**Saa mbili**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**

*Karatasi hii ina sehemu mbili; A na B.*

*Jibu maswali mawili ukichagua moja kutoka kila sehemu.*

*Swali la ziada halitasahihishwa.*

*Majibu yote yaandikwe kwenye kijitabu ulichopewa.*

## SEHEMU A

### UANDISHI WA INSHA

#### Ama

1. Umemaliza mitihani ya kidato cha nne katika shule ya upili ya Safari Sawa S.L.P 321, Kasambya, na kurudi nyumbani. Nyumbani kwenu, baba yako huwa analeta magazeti kila jioni anapotoka kazini. Siku moja ukiwa nyumbani unaamua kupitia gazeti la New Vision ambamo huwa wanatangaza kazi za aina mbalimbali. Unapokuwa ukisoma, unagundua tangazo la kazi ya msaidizi wa karibu wa mkuu wa shule yenu afisini mwake. Unaona ni bora uchangamkie fursa hiyo kwa kuwasilisha maombi. Andika utakayowasilisha. *(Tumia Maneno kati ya 180 – 200)*

#### Au

2. Umefaulu mitihani ya kidato cha nne na kujiunga katika kidato cha tano katika shule hiyo hiyo. Kwa kuwa wewe ulikuwa kiongozi ukiwa katika kidato cha tatu na ukapata uzoefu na umaarufu, umeamua kugombea kiti cha kiranja mkuu wa shule. Kampeni za toka nitoke zimefanyika na umeibuka mshindi. Shuleni kumeandaliwa siku ya kuapisha viongozi wapya itakayohudhuriwa na wazazi wa wale waliopata ushindi. Wazazi wako wamehudhuria siku hiyo wakiwa na furaha kubwa. Wewe uliyechaguliwa kama kiranja mkuu utaapishwa kwanza na kutarajiwa kuzungumza kwa hadhira. Andika utakayowasilisha. *(Tumia Maneno kati ya 200 – 220)*

## SEHEMU B

### UFUPISHO

3. *Kumekuwa na mkutano kuhusu usalama ambapo Jenerali Karimu ameeleza mengi kuhusu ukosefu wa usalama na athari zake. Uliweza kuhudhuria mkutano huo na kuelewa kila jambo lililoelezwa. Taarifa nzima imeandikwa hapa. Iandike tena kwa ufupi ukitumia maneno 80.*

Siku hiyo, ndipo wanafunzi wengi tulitambua kwamba kuna mengi yaliyokuwa yametokea kabla ya kuzaliwa kwetu. Huku tukiendelea kuchora picha akilini, kila mtu alikuwa amenyamaza na kutulia tuli kama maji mtungini!

Jenerali Karimu ambaye ni mhamasishaji, mtendaji wa haki za binadamu, aliendelea kutusimulia hali ya amani na usalama ilivyokuwa nchini wakati alipokuwa kijana. "...Wakati huo, tulikuwa hatuwezi kutembea wakati wa usiku. Waliotembea usiku, wangechapwa viboko na kuporwa kila kitu. Aliyenusurika kuuawa, wakati mwingine wangemwachia mavazi ya ndani tu kuziba utupu wake! Wizi ulikuwa umezidi, mauaji ya kila siku yaliwaacha mayatima wengi bila uwezo wa kusukuma maisha. Wafanya biashara wengi waliamua kuacha kazi kwa kukosa usalama. Hata hivyo, hakukuwa na urekebishaji wala ujenzi wa barabara, hospitali, shule kwa sababu ya ukosefu wa usalama. Bunduki kumilikiwa na wananchi wa kawaida lilikuwa tishio kubwa kwa maisha ya wananchi. Jambo la wananchi kumiliki bunduki lilisababisha hofu kubwa kwa wananchi wenyewe.

Nchini kulikuwa na shida ya ukosefu wa kazi kwa vijana. Wale wachache waliopata kazi, wangukuwa ndugu au marafiki wa wale waliokuwa madarakani. Kwa hivyo, vijana wengi wangeanzisha migomo na maandamano ambayo yangeishia katika mapigano na kuharibu mali za watu. Walioshikwa na maafisa wa ulinzi wa serikali katika maandamano hayo, wakati mwingi wangepigwa, wengine wangelemazwa na hata wengine wasionekane tena.

Pia, ukosefu wa kazi ungesababisha vijana kuunda makundi ya waasi na magaidi. Ungesikia kwamba mabomu yalilipuka usiku na kuua watu katika sehemu mbalimbali. Kuna wakati ungesikia redioni kuwa waasi wamevamia kijiji au shule fulani, wamebaka wanawake, wamewateka nyara vijana na kuwashirikisha katika makundi yao, wengine mifugo yao inachukuliwa, nyumba za wananchi kuchomwa bila sababu."

Jenerali aliendelea kutueleza jinsi mambo yalivyobadilika baada ya mapinduzi. "Serikali mpya ilichukua uongozi na kuanzisha mipango ya kupata amani na usalama. Kwanza, wananchi walishirikishwa katika kuripoti visa vya uhalifu, pia kuhimiza demokrasia na kuiombea nchi na kuweka taasisi za kuchunguza mafisadi.

Vile vile, serikali imeanzisha shule za ufundi ili vijana waweze kujiajiri. Utawala mzuri umehakikisha usalama. Hayo yote yamewezesha serikali kutoa huduma bora kama vile barabara safi, hospitali, shule, usambazaji wa umeme pamoja na njia za kisasa za mawasiliano, hali ambazo zimesaidia sana katika maendeleo ya nchi."